



# **KIBABII UNIVERSITY**

## **UNIVERSITY EXAMINATIONS**

**2020/2021 ACADEMIC YEAR**  
**THIRD YEAR FIRST SEMESTER**

**MAIN EXAMINATION**

**FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)**

**COURSE CODE: SWA 313**

**COURSE TITLE: MBINU ZA UFUNDISHAJI WA KISWAHILI**

**DATE: 23/07/2021**

**TIME: 9:00AM-11:00AM**

---

### **MAELEKEZO**

Jibu maswali **matatu** pekee.

Swali la Kwanza ni la **lazima**

**MUDA: Masaa Mawili (2)**

## Maswali

1. (a) Tofautisha dhana ya 'masuala ibuka' na 'udhibiti wa darasa' katika silabasi ya Kiswahili ya mwaka 2002. (alama 4)
- (b) Fasili dhana zifuatazo jinsi zinavyotumika katika elimu ya lugha. (alama 6)
  - i. Lugha ni tata
  - ii. Lugha ni kamilifu
  - iii. Ala ya upataji wa lugha
- (c) Hivi karibuni Chomsky amerejelea ala ya upataji lugha kama Sarufi ya Kimajumui. Sarufi hii ina kanuni ambazo hupatikana katika lugha zote za binadamu. Bainisha ithibati ambazo Chomsky anatoa kutetea mtazamo huu. (alama 8)
- (d) Mbali na kuwa na uelewa wa somo lake, kujimudu na kujiweka katika nafasi ya wanafunzi wake ili kutimiza mahitaji yao ya kielimu, fafanua sifa ambazo mwalimu anayefundisha somo la lugha ya Kiswahili anafaa kuwa nazo. (alama 12)
2. Umejiriwa kufunza Kiswahili kwa wanafunzi wasiozungumza Kiswahili kama lugha yao ya kwanza. Fafanua kanuni zozote utakazozingatia darasani unapofundisha lugha hii ukiegemea nadharia yoyote ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili. (alama 20)
3. Mwalimu anayefundisha lugha ya pili anaweza kutumia njia moja au mseto wa njia kadhaa kuwafundisha wanafunzi wake. Pambanua nne kati ya njia hizo. (alama 20)
4. (a) "Ili kuainisha nyenzo, tunaweza kutumia vigezo viwili. Kigezo cha hisia zinazoathirika na kigezo cha uhalisia wa nyenzo zenyewe" (Kawoya, 1988). Onesha aina za nyenzo kwa kuzingatia vigezo hivyo viwili. (alama 10)
- (b) Fafanua madhumuni ya uandalizi wa ratiba ya somo. (alama 10)
5. Bainisha umuhimu wa usetaji katika kufundisha Kiswahili. (alama 20)